**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# BENKI KUU YA TANZANIA

**4 Julai 2024**

## TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA

**Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania, imeamua Riba ya Benki Kuu (CBR) kuendelea kuwa asilimia 6 kwa robo mwaka itakayoishia Septemba 2024.** Uamuzi huu umefikiwa katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 3 Julai 2024. Tathmini ya Kamati kuhusu mwelekeo wa uchumi na vihatarishi mbalimbali inaonesha kwamba, utekelezaji wa sera ya fedha kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024 umefanikiwa kudhibiti mfumuko wa bei na kubaki chini ya lengo la asilimia 5. Maamuzi ya Kamati pia yanazingatia mtazamo chanya wa uchumi wa dunia, ambapo matarajio ni kuendelea kupungua kwa mfumuko wa bei katika nchi nyingi, kuimarika kwa ukwasi katika masoko ya fedha duniani, na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Aidha, Kamati inatarajia uchumi wa ndani kuendelea kukua kwa kasi, sanjari na upatikanaji wa chakula cha kutosha, na kupungua kwa kasi ya kushuka kwa thamani ya shilingi kufuatia ongezeko la mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii, pamoja na mauzo ya dhahabu na mazao ya biashara na chakula.

Katika kutathmini mwenendo wa uchumi wa dunia, Kamati ilibaini kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi nyingi kwa robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2024. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua, sanjari na kuimarika kwa ukwasi katika masoko ya fedha duniani, na benki kuu katika nchi nyingi kuanza kupunguza viwango vya riba. Bei ya mafuta ghafi ilipungua, licha ya kuongezeka kidogo mwishoni mwa mwezi Juni 2024. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa juu, ikiashiria dhahabu kuendelea kutumika kama uwekezaji mbadala katika mazingira ya kushuka kwa thamani ya sarafu mbalimbali na migogoro ya kisiasa duniani. Matarajio ni uchumi wa dunia kuendelea kuimarika katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2024 na 2025, licha ya kuwepo kwa hatari ya kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa na mizozo ya kibiashara.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa Tanzania, Kamati imeridhishwa na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, kutokana na utekelezaji wa sera thabiti na maboresho mbalimbali yenye lengo la kukuza uchumi. Hali hii ya kuimarika kwa uchumi inatarajiwa kuendelea katika siku zijazo, kufuatia hali nzuri ya hewa kwa ajili ya shughuli za kilimo, upatikanaji wa uhakika wa umeme, uboreshaji wa miundombinu (hususan reli, barabara, na bandari), pamoja na sera na programu za maboresho. Baadhi ya maeneo mahsusi ya mwenendo wa uchumi yaliyofanyiwa tathmini na Kamati ni kama ifuatavyo:

(i) Uchumi ulikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2023, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, uchimbaji madini na mawe, ujenzi na shughuli za kifedha (hususan ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi). Aidha, shughuli za utalii, ambazo zinategemeana na sekta nyingine za uchumi zimeendelea kuchangia kuimarika kwa uchumi nchini. Kamati inakadiria ukuaji wa uchumi kuwa takriban asilimia 5 na 5.4, katika robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2024, mtawalia. Vilevile, mwenendo wa uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa imara, ambapo ulikua kwa asilimia 7.4 mwaka 2023, ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2022. Mwenendo huu unachangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za utalii, huduma za chakula na uwekezaji kwenye sekta ya ujenzi. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi nchini unatarajiwa kuendelea katika nusu ya pili ya mwaka 2024 na 2025.

(ii) Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu na chini ya lengo la nchi la asilimia 5, na vigezo vya utangamano vya kikanda kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Mwezi Aprili na Mei 2024, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3 na 3.1, mtawalia. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa mfumuko wa bei wa chakula kufuatia uwepo wa chakula cha kutosha nchini, pamoja na sera thabiti za fedha na bajeti. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei umeendelea kupungua hadi kufikia takriban asilimia 5, kutokana na kupungua kwa bei za chakula na bidhaa zisizo za chakula. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3-4, katika nusu ya pili ya mwaka 2024 na kuendelea, ikichagizwa na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, upatikanaji wa chakula cha kutosha, upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme, na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

(iii) Kuendelea kuimarika kwa hali ya uchumi, kumechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji imara wa mikopo kwa sekta binafsi na utulivu wa sekta ya fedha. Katika robo ya pili ya 2024, mikopo ya sekta binafsi inakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 16.4 ikilinganishwa na asilimia 17.1 katika robo iliyotangulia. Sekta ya benki iliendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha huku ikitengeneza faida. Aidha, amana, rasilimali na mikopo imeendelea kuongezeka. Ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika, kufuatia kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu hadi asilimia 4.4 Mei 2024, ndani ya wigo unaokubalika wa chini ya asilimia 5, na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Mikopo kwa sekta binafsi inatarajiwa kuendelea kuongezeka katika kipindi kijacho cha mwaka 2024 kutokana na kuimarika kwa hali ya uchumi wa dunia na wa ndani.

(iv) Utekelezaji wa bajeti ya Serikali umeendelea kuwa wa kuridhisha huku ukichagiza utekelezaji wa sera ya fedha. Mapato ya ndani kwa Tanzania Bara yanakadiriwa kufikia asilimia 95 ya lengo. Kwa upande wa Zanzibar, mapato yanakadiriwa kuvuka lengo kwa asilimia 0.3 kutokana na maboresho katika usimamizi wa kodi na kuongezeka kwa utayari wa wananchi kulipa kodi. Katika mwaka 2024/25, Serikali inakusudia kutekeleza sera

inayolenga kupunguza matumizi na kuendelea kutekeleza programu ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya *Extended Credit Facility (ECF)*, pamoja na programu ya *Resilience and Sustainability Facility (RSF)*.

(v) Urari wa malipo ya kawaida uliendelea kuimarika, kuendana na kupungua kwa athari za mitikisiko ya kiuchumi duniani. Mauzo nje ya nchi yaliongezeka kutokana na uuzaji wa dhahabu, mazao asilia na shughuli za utalii. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje uliongezeka japo kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mauzo ya nje. Hivyo, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida (current account deficit) inakadiriwa kupungua hadi dola milioni 959.2 katika robo inayoishia Juni 2024 ikilinganishwa na dola milioni 977.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo ya kawaida unakadiriwa kuwa ziada ya dola za Marekani milioni 421.5 katika mwaka unaoishia Juni 2024, ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 411.5 katika kipindi sawia cha mwaka 2023. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma, hususan utalii. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kuendelea kupungua hadi asilimia 3.2 ya Pato la Taifa katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2024.

(vi) Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha kwa kuwa na zaidi ya dola za Marekani bilioni 5, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa zaidi ya miezi 4. Upatikanaji wa fedha za kigeni uliimarika kiasi, mwishoni mwa mwezi Juni 2024, kutokana na ongezeko la fedha za kigeni kutoka kwenye mauzo ya tumbaku, dhahabu na shughuli za utalii. Matarajio ni kuongezeka zaidi kwa fedha za kigeni nchini kupitia mapato yatokanayo na shughuli za utalii, mauzo ya madini, bidhaa asilia, na usafirishaji wa chakula kwenda nchi jirani. Matarajio ya kuimarika kwa hali ya uchumi wa dunia na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia pia yatachangia ongezeko hilo. Aidha, Benki Kuu inatarajiwa kuongeza akiba yake ya fedha za kigeni kupitia ununuzi wa dhahabu kutoka katika masoko ya ndani.

**EMMANUEL M. TUTUBA**
**GAVANA**